

# DARUBINI

## Sera ya Ushirikishwaji Wazawa Sekta ya Madini: Maendeleo na Changamoto Zilizopo.

Toleo la 2
Septemba 2023

Imedhaminiwa na: Belgium partner in development

Imechapishwa na:
International Peace Information Service (IPIS), HakiRasilimali,
Business Human Rights Tanzania(BHRT) & Avocats Sans Frontiéres(ASF)

# Sera ya Ushirikishwaji Wazawa Sekta ya Madini: Maendeleo na Changamoto Zilizopo.

Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali za madini, Tanzania imekuwa na mafanikio katika sekta ya madini kwa miaka mingi, ingawa kwa kipindi kirefu kumekuwa na wasiwasi kuhusu ushirikishwaji hafifu ambao unapelekea manufaa machache kwa wazawa. Kutokana na wasiwasi huu, Tanzania imeanzisha ilianzisha sera Ushirikishwaji wazawa sekta ya madini ya mwaka 2018, ili kuhakikisha faida zitokanazo na shughuli za madini zinagawanywa kwa usawa kwa wananchi. Makala hii inaongelea maendeleo na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa sera ya madini nchini Tanzania.

## Ushirikishwaji wa wazawa una umuhimu gani katika sekta ya madini?

Kwenye Dira ya nchi ya mwaka 2025, Tanzania inatarajia kuhamia kwenye uchumi wa viwanda uliojikita kwenye rasilimali. Dira hii imeweka bayana umuhimu wa kuhakikisha ushirikishwaji wa wazawa kwenye mabadiliko ya uchumi kupitia maliasili, ili kuongeza manufaa na maendeleo kwa nchi na wazawa. Hivyo basi ushirikishwaji Chanya wa wazawa sharti uhusishe uwezekano wa wananchi kujipatia ajira, mafunzo, masoko ya bidhaa na huduma zao ikiwa ni pamoja na kushiriki katika kuongeza thamani mazao ya madini. (Oliver, 2021) njia pekee ya kufikia haya malengo ni kwa kuiwezesha jamii kupitia ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta.

Nchini Tanzania, sera za utaifa wa rasilimali zilianzishwa mwaka 2017 kudhibiti tasnia ya uziduaji kwa lengo kuu la kuhakikisha kuwa nchi itaongeza manufaa yake kutokana na shughuli za uziduaji. (Jacob, 2018). Mojawapo ya mikakati katika muktadha huu ni uundaji wa sera ya ushirikishwaji wazawa. Kupitia sera hizi makampuni ya kitanzania na watanzania wanapewa kipaumbele katika mnyororo wa thamani wa uziduaji, ili kuwaruhusu kukamata kodi kubwa za kiuchumi (Djeynaba, 2021), kupitia ajira, fursa za mafunzo, na kupata mikataba ya kusambaza bidhaa na huduma kwenye sekta hiyo (Oliver, 2021).

Umuhimu wa kuendeleza ushirikishwaji wa wazawa, hasa katika ngazi ya chini, unaweza kueleweka vyema kwa kuzingatia madhara hasi yanayotokana na uchimbaji wa madini. Madhara ya uchimbaji madini, kama vile kuhamishwa, uchafuzi wa maji na hewa, huathiri vibaya jamii zinazoishi karibu na maeneo ya uchimbaji madini (Prakash, 2022). Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya kufidia jamii zilizoathiriwa. Mojawapo ya njia za kufanikisha hili ni kuwezesha ushiriki wa jamii katika sekta kupitia kuendeleza ushirikishwaji wa wazawa.

## Mfumo wa Udhibiti wa Mahitaji ya ushiriki wa wazawa katika Sekta ya Madini Tanzania

Nchini Tanzania, Sera na Sheria zinazoongoza sekta ya madini zimepitiwa upya ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanapewa upendeleo katika ajira na usambazaji wa bidhaa na huduma katika sekta hiyo. Sheria hizo ni Pamoja na sheria ya madini sehemu ya 123 ya mwaka 2019, sheria ya utajiri asili (mamlaka ya kudumu ya nchi) ya mwaka 2017, na ya utajiri wa asili (mapitio na majadiliano kuhusu masharti hasi) ya mwaka 2017 ikiwa Pamoja na kanuni zake kama ile kanuni ya uchimbaji wa madini (ushirikishwaji wa wazawa) ya mwaka 2018. Uchimbaji wa madini (usindikaji wa madini), uchimbaji wa madini (uongezaji wa thamani) na ile kanuni ya uchimbaji wa madini (kiwango cha chini cha hisa na uuzaji wa hisa kwa umma) ya mwaka 2016 kama zilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.

Sheria na kanuni husika hujadili vipengele kumi na moja (11) tofauti vya mahitaji ya ushirikishwaji wa wazawa (HakiRasilimali, 2023). Hizi ni pamoja na wajibu wa kampuni kuwasilisha mpango wa ushirikishwaji wa wazawa, unaoeleza kwa kina mipango, taratibu na fursa kwa raia wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani wa madini. Sera za ushirikishwaji wa wazawa zinalazimisha zaidi makampuni kutoa kipaumbele cha kwanza kwa manufaa na huduma zinazotolewa na Watanzania na kutofanya hivyo kunaweza kusababisha kunyang'anywa leseni zao.

## Ushirikishwaji wa Wazawa Nchini Tanzania

Licha ya sheria na kanuni zilizopo, hadi sasa tafiti zilizopo kuhusu ushirikishwaji wa wazawa, zinaonyesha kuwa kuna ushahidi mdogo kwamba sera ya ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini nchini Tanzania imetoa manufaa ya ushindani kwa wenyeji (Weldegiorgis, 2021) na kuongeza manufaa yanayotokana na madini husuani katika ngazi ya jamii (Kinyondo, 2019).

Utekelezaji wa sera za ushiriki wa wazawa katika uchimbaji madini hukumbana na aina mbalimbali za changamoto. Mojawapo ya changamoto kubwa iko katika tofauti kati ya ujuzi unaohitajika na nguvu kazi inayopatikana. Lengo la sera ya kuongeza ajira za ndani linakumbwa na uhaba wa watu wenye ujuzi kwa ajili ya majukumu maalumu ndani ya sekta ya madini. HakiRasilimali, 2023 iligundua kuwa ajira katika migodi mikubwa bado hazipatikani kwa wenyeji wengi. Ikisababishwa na ukosefu wa ujuzi, na hata sifa zinazohitajika kwa maana hiyo Kuziba pengo hili la ujuzi kunahitaji utekelezaji wa mafunzo endelevu na mipango ya elimu.




Licha ya hivyo, makampuni ya ndani yamekuwa na uwezo hafifu kwa sababu Makampuni haya mara nyingi hukosa ustadi unaohitajika wa kiufundi, kifedha, na vifaa vya kushindana na wenzao wa kimataifa, na hivyo kukosa uwezo wa kushindana. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa wazawa wanahitaji usaidizi wa kupata kandarasi za usambazaji. Hata hivyo, wachache wanaobahatika kupata, mara nyingi huishia kusambaza bidhaa za thamani ya chini kama vile mbogamboga na matunda.

Aidha, utekelezaji wa sera hizi bado unakumbwa na changamoto. Baadhi ya makampuni ya uchimbaji madini yanaweza kutafuta njia za kukwepa masharti ya sera, yakisisitiza hitaji la mifumo thabiti ya udhibiti na ufuatiliaji. Zaidi ya hayo, miundombinu duni huleta tatizo katika baadhi ya maeneo ya uchimbaji madini. Licha ya juhudi za uwekezaji, bado kuna upungufu katika huduma muhimu kama vile umeme unaotegemewa, usambazaji wa maji na kadhalika, mapungufu haya yanaathiri ufanisi wa jumla wa sera katika kuinua jamii ya wazawa.

Kwa hakika, changamoto zinazozunguka utekelezaji wa sera za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini zina mambo mengi. Changamoto hizi ni pamoja na vikwazo katika uwezo wa makampuni ya ndani, taratibu za uzingatiaji, swala la ujuzi na miundombinu. Hivyo basi kukabiliana na changamoto hizi ni muhimu kuwepo na ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya sera ya uwezeshwaji wazawa ndani ya sekta ya madini.

Licha ya changamoto zilizopo, kuna mafanikio makubwa yamepatikana katika kukabiliana na matatizo hayo katika siku za hivi karibuni. Mnamo Machi 16, 2023, wakati wa Kongamano la Pili la Ushiriki wa Tanzania katika Sekta ya Madini lililofanyika Arusha, mfumo wa ushirikishwaji wa wzawa Ndani ya Tanzania na Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) ulizinduliwa rasmi na Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa. Katika hotuba yake, Dk. Kiruswa alibainisha mafanikio makubwa yaliyotokana na maboresho ya Sheria ya Madini na Kanuni za ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za ajira, uanzishwaji wa programu za mafunzo kwa Watanzania, na kuongezeka kwa matumizi ya huduma na bidhaa zinazotolewa na Watanzania. Katika hotuba yake Bw. Kiruswa alibainisha kuwa, fursa za ajira kwa Watanzania katika migodi mikubwa zilipanda kutoka 6,668 mwaka 2018 hadi 15,341 mwaka 2022. Aidha, Watanzania 8,066 walipata mafunzo katika sekta ya madini mwaka 2022, na kugharimu Shilingi za Kitanzania bilioni 3.4 (takriban Euro milioni 1.2). Maboresho haya yanaweza kuhusishwa na uhamishaji wa ujuzi na teknolojia chini ya Sera ya ushirikishwaji wa wazawa ambayo inazitaka kampuni za madini kuwekeza katika mafunzo na kuendeleza ujuzi wa wafanyakazi wa Tanzania. Kwa hiyo, wafanyakazi wa ndani wanapata uzoefu na ujuzi muhimu, kuchangia maendeleo kama nguvu kazi ya nchi na kuimarisha uhamisho wa teknolojia kwenye sekta ya madini ndani ya nchi.

Mafanikio mengine yaliyotajwa na Naibu Waziri Kiruswa ni pamoja na kuongezeka kwa manunuzi ya ndani, ambayo ni dola bilioni 2.22, sawa na asilimia 97.4 ya ununuzi wa makampuni ya madini mwaka 2022, yaliyofanywa kupitia makampuni ya Kitanzania ikilinganishwa na dola milioni 238.71 sawa na asilimia 46 mwaka 2018. Watoa huduma waliongezeka hadi 1,386 mwaka 2022, kutoka 623 mwaka 2018, ikiwa ni ukuaji wa 81%. (Tume, 2023) Hii imesababisha kukua kwa biashara za ndani, kwani sasa wanaweza kutoa pembejeo muhimu kwenye sekta ya madini na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

## Kuelekea Maendeleo ya kweli ya Ushirikishwaji Wazawa Sekta ya Madini.

Utekelezaji wa Sera ya ushirikishwaji wa wazawa nchini Tanzania umeonyesha matokeo mazuri katika kukuza ushiriki wa wazawa na maendeleo ya kiuchumi katika sekta ya madini.

Hata hivyo, changamoto kama vile vikwazo kwenye uwezeshaji, ushirikishwaji na upungufu wa miundombinu zinahitaji uangalizi, na ushirikiano endelevu miongoni mwa wadau ili kuhakikisha ufanisi wa sera na kufikia malengo yake ya muda mrefu, Kuendelea kufuatilia na kuboresha sera ni muhimu ili kuongeza matokeo chanya ndani ya nchi. Ili kuimarisha ushirikishwaji wa wazawa, ni muhimu mafunzo yatolewe kwa wadau ili waweze kuelewa umuhimu wa ushirikishwaji wa wazawa kwenye ngazi ya kitaifa na mashinani. Ni muhimu pia kuondoa vikwazo vyote dhidi ya ajira kwa wazawa na kuwapa mafunzo maalumu ili waweze kuliingia soko la bidhaa na huduma katika sekta ya madini. Licha ya hivyo tume ya madini inapaswa kusimamia utekelezaji wa sheria ya ushirikishwaji wa wazawa kikamilifu.




"Baadhi ya makampuni ya madini ya kigeni bado yanakataa kutumia bidhaa na huduma maalum zinazozalishwa na wakazi wa ndani nchini Tanzania, kwa kutumia ubora kama uhalali. Bila mpango madhubuti wa kuimarisha uwezo wa wenyeji, juhudi zetu za kukuza ushiriki wa wazawa zitaendelea kuwa duni kwa muda mrefu" .

Prof. Abel Kinyondo
University of Dar es Salaam.

# Sauti za Jamii: ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini Tanzania: maoni toka kwenye sauti za Dhahabu za Geita na Mara.

Mwanzoni mwa mwaka 2023, utafiti wa kina uliofanywa na HakiRasilimali ulitoa mwanga juu ya suala kubwa ambalo limedumu kwa muda mrefu katika maeneo yenye rasilimali nyingi nchini Tanzania na sera ya ushiriki wa wazawa katika sekta ya madini. Kwa kuangalia maeneo ya dhahabu ya Geita na Mara, utafiti ulilenga kukusanya maoni ya wananchi kuhusu utekelezaji wa Kanuni ya Madini (Ushirikishwaji wa wazawa) ya mwaka 2018.

Utafiti ulibaini kwamba ushirikishwaji wa wazawa katika ngazi ya chini umekuwa duni, fursa zinazoendelea kupotea kwa wazawa zinasababishwa na kutotekelezwa kwa sera ya kushirikisha wazawa. Ikiwa ubaguzi na ukosefu wa uwazi ndiyo vyanzo kuu vya kutokuwepo kwa fursa kwa wazawa, mhojiwa mmoja akilalamika anasema "Tumeona maombi yanawekwa kwenye mbao za matangazo za ofisi ya kijiji na watoto wetu hapa wanaomba kazi hizo lakini kwa miaka mingi hatujaona watoto wetu wakifanikiwa kupata kazi hiyo, tunaona tu watu kutoka nje ya Nyamongo wakipata ajira".

Utafiti ulifichua pia kuwa, wakati baadhi ya wenyeji walifanikiwa kushiriki katika mnyororo wa thamani wa migodi, mara nyingi walijikuta wakitoa bidhaa za thamani ya chini kama mboga na matunda. Zaidi ya hayo, fursa hizi chache zilipatikana mara kwa mara kupitia miungano, vikwazo vya kifedha, kutoaminiana, hukwamisha sana ushiriki wa mtu binafsi.

Na Jambo la kushangaza ni kwamba kucheleweshwa malipo kwa muda mrefu kutoka kwa makampuni ya madini yaliibuka kama kikwazo kikuu, na kukandamiza mzunguko wa biashara wa wasambazaji hawa wa ndani. Kama ilivyoelezwa wazi na mhojiwa mmoja "Tuna zabuni ya kusambaza mboga na matunda katika Mgodi wa Dhahabu wa North Mara kupitia AKO Group Ltd, kwa kawaida tunasambaza mboga na matunda kwa wakati, lakini tunakabiliwa na changamoto ya malipo kucheleweshwa jambo ambalo linakwamisha mzunguko wa biashara kwa sababu tunashindwa kununua vifaa vingine vinavyohitajika kwa uzalishaji mwingine".

Utafiti huu ulifichua pengo la kutatanisha katika Nyanja ya ushirikishwaji wa wazawa na uliambatana na madai kwamba makampuni ya uchimbaji madini yamefumbia macho kazi muhimu ya kuwezesha jamii kupitia mafunzo muhimu. Kwa upande mwingine uelewa wa ushirikishwaji wa wazawa kwenye ngazi ya kitaifa na mashinani ni changamoto na hivyo kusisitiza hitaji la dharura la kampeni za kina za uhamasishaji ili kufafanua umuhimu wa ushirikishwaji wa wazawa.

Hata hivyo kulingana na tafiti wananchi wengi wana wasiwasi juu ya serikali katika kutekeleza sera ya ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini Athari za mashaka haya yanapingana vikali dhidi ya Tume ya Madini, ambayo inabeba jukumu la kusimamia maendeleo ya sera ya ushiriki wa wazawa nchini Tanzania. utafiti wa HakiRasilimali unatumika kama mwito mkubwa wa kuoanisha sera na utekelezaji, kuhakikisha fursa za uchimbaji kwa wazawa zinatekelezwa kwa usawa.




**"Moja ya changamoto kubwa inayokabili vikundi vya wanawake wakati wanapokea mikopo kutoka kwa serikali za mitaa ni kiwango duni cha ulipaji, mara nyingi kutokana na vikundi kubadilisha malengo ya awali ya mkopo. Changamoto nyingine ni kiwango kidogo cha ushiriki na mwitikio katika kuhudhuria vikao vya mafunzo na semina."**
**Valeria Makonda:**
**Afisa Maendeleo ya Jamii: Geita TC**

## Habari kwa Ufupi: Hadithi zaidi kuhusu ushiriki wa wazawa katika sekta ya Madini nchini Tanzania.

1. Serikali kuongeza nguvu kwenye swala la ushiriki wa wazawa kwenye sekta ya Madini: (IPP Media)
2. Maisha ya Geita yanabadilishwa na miradi ya kijamii na kiuchumi inayoongozwa na GGML: (Daily News)
3. Matokeo yasiyotarajiwa: Tatizo ushiriki wa wazawa, Barrick:(Daily News)
4. Dk. Kiruswa azindua mkakati wa ushiriki wa wazawa, kwa ajili ya ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini: (Tume, 2023)
5. Wadau Wadai Ushirikishwaji Wenye tija kwa Jamii Katika Uendeshaji Madini: (Policy Forum)
6. Watafiti: "jamii ipewe kipaumbele katika ushiriki kwenye sekta ya madini" (Sunday News Newspaper: 2nd July 2023)
7. Jinsi Tanzania inaweza kukuza ushiriki wa wazawa: (The Citizen)
8. Ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini Tanzania: maoni toka kwenye sauti za dhahabu za Geita na Mara. (HakiRasilimali, 22023)




**Novemba!**

**Chapisho linalofuata litachapishwa mnamo Novemba 2023, uchapishaji utakuwa juu ya haki za binadamu na upatikanaji wa suluhu katika sekta ya uziduaji.**

IPIS · HakiRasilimali — Enhancing Transparency & Accountability of the Extractive industry in Tanzania · BHRT · ASF Avocats Sans Frontières